

Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA**

Wafugaji wapongezwa kurejesha mkopo kwa wakati

**Na Marco Maduhu,
KISHAPU**

OFISA Maendeleo ya Jamii wilayani Kishapu, Abednego Madole, amekipongeza kikundi cha wafugaji cha umoja ni nguvu kilichopo katika Kijiji cha Beledi kwa kufanikiwa kurejesha mkopo wa Sh.milioni 4.3 ambao walipatiwa na halmashauri.

Alitoa pongezi hizo juzi

wakati wa halfa ya kukabidhi ng'ombe wengine kwa wanakikundi hao.

Madole alisema kikundi hicho ni mfano wa kuigwa kwa sababu baadhi ya vikundi ambavyo vimepewa mkopo na halmashauri vimekuwa vikisuasua kurejesha marejesho na kufikia hatua ya kupelekana mahakamani.

"Hongereni sana wanakikundi kwa hatua mliyofikia

mmekuwa mfano kwa vikundi vingine, jambo la kumaliza kurejesha mkopo ni jambo kubwa sana, hii inaonyesha ni jinsi gani mlivyo na uwezo wa kujisimamia, Halmashauri ipo tayari kuendelea kushirikiana na nyie kupitia Ofisi ya Maendeleo ya Jamii," alisema.

Katibu wa kikundi hicho, Nkuba Shija Masebo, alisema kwamba kikundi kilianza na mtaji wa Sh.75,000 baada ya

hapo walipata mkopo wa Sh. milioni 4.3 kutoka halmashauri ambao uliwasaidia kununua mbuzi 42 na hadi sasa kikundi kina mbuzi 192 na ng'ombe tisa.

Alisema kikundi hicho baada ya kurejesha mkopo wote sasa kimebaki na faida ya Sh.800,000 fedha ambazo watazitemia kuendelea mtaji katika kikundi chao na kuinuka kiuchumi.

Wenye mabucha waonywa tabia kubeba nyama begani

Na Peter Mkwavlla, DODOMA

WAHUDUMU wa bucha za nyama jijini Dodoma wametakiwa kuacha tabia ya kubeba nyama mabegani, badala yake watumie vyombo maalumu vinavyostahili ili kulinda afya za walaji. Mkurugenzi wa Kampuni ya Talibo Traders Company LTD inayojihusisha na uzaji wa nyama pori jijini hapa, Nelson Talibo alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu usalama wa nyama katika bucha.

Aidha, aliwataka wahudumu hao wa mabucha kupima afya zao mara kwa mara ili kujilinda na maambukizi ya magonjwa yanayoweza kuwapata wao pamoja na watumiaji wa nyama hizo.

Mkurugenzi huyo aliwataka pia wahudumu hao kutumia vyombo vya kisasa vya kubeba nyama badala ya kutumia mabega na kujitwisha vichwani kwa kuwa hali hiyo inaweza kusababisha kwa asilimia kubwa kuwepo kwa maambukizi ya magonjwa kwa pande zote mbili.

"Wahudumu walio wengi nyama zinapoletwa kwenye mabucha baadhi yao badala ya kubebea kwenye vyombo vya kisasa vinavyostahili wanatumia mabega na vichwa vyao kubebea nyama hizo hali ambayo ni hatari kiafya," alisema.

Hata hivyo, aliwataka walaji wa nyama kujihadhari na matumizi ya nyama zinazouzwa mitaani kwa kuwa zilizo nyingi zimekosa vigezo kutokana na kuchinjwa bila kupimwa na wataalamu wa afya.

Hata hivyo, aliwaomba wamiliki wa mabucha kuhakikisha wanajipanga kiafya kwenye maeneo yao, hii ni pamoja na wafanyakazi kuwa na sare na wanapimwa afya kwa lengo la kujilinda na maambukizo ya magonjwa.